



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO

Samora, Avenue, ExTelecoms House, 2nd Floor, P.O Box 4273, Dar es Salaam, Tel: +255222129868/74, Fax: +255222129878,
General eMail: info@ega.go.tz, CEO eMail: ceo@ega.go.tz, Website: www.ega.go.tz



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) imeaanda utaratibu mahususi wa kutembelea wateja wake ambao ni taasisi za umma ili kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali zinazotokana na huduma inazozitoa.

Huduma hizo ni pamoja na Mfumo wa Barua Pepe Serikalini unaorahisisha mawasiliano ndani ya Serikali, Uhifadhi wa mifumo na tovuti za Serikali, Mfumo wa utoaji huduma kwa Simu za Mkononi kupitia ***152*00#**, Uratibu wa Mtandao wa Serikali, Ugawaji wa Masafa ya Internet, Huduma ya ujumbe mfupi wa Maandishi (sms), Utengenezaji wa mifumo na tovuti na usajili wa anuani za tovuti.

Utaratibu huu ni sehemu ya maadhisho ya Wilki ya Utumishi wa Umma ambayo hufanyika kila mwaka kuanzia tarehe 16 hadi 23 Juni na **Kaulimbiu** kwa mwaka huu ni: **Uongozi wa umma kwa ukuaji jumuishi; kuelekeea katika Afrika tunayoitaka.**

Hivyo, katika kutimiza agizo la Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Mhe. Angella Kairuku, Wakala imepanga kutembelea baadhi ya taasisi za umma **34** zilizopo Dar es Salaam zinazopata huduma mbalimbali za wakala kwa siku mbili tarehe 22 na 23 Juni, 2016.

Taasisi zitakazotembelewa tarehe 22 juni 2016 ni pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maendeleo na Makazi, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundii, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa.

Nyingine ni Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA), Ofisi ya Bunge iliyopo Dar es Salaam, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGEN), Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima (TIO), Mahakama ya Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA),

Siku ya pili ya tarehe 23 Juni 2016 taasisi zitakazotembelewa ni Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ya

Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), Kampuni ya Reli Tanzania (TRL), Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS).

Nyingine ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora (NHBRA), Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Wakala wa Usajili na Utoaji wa Leseni za Biashara (BRELA), na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA).

Kila taasisi itatembelewa na wataalam wawili wa Wakala watakaosikiliza maoni na kutoa msaada wa kiufundi na ushauri wa kitalaam katika kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza juu ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Wakala.

Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa mwaka 2012 kwa sheria ya Wakala za Serikali Na. 30, Sura ya 245 ya mwaka 1997. Wakala hii ina majukumu na mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini Tanzania

xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx xxx**MWISHO**xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx

Imetolewa Na:

SUZAN MSHAKANGOTO

MENEJA HABARI, ELIMU NA MAWASILIANO

WAKALA YA SERIKALI MTANDAO (eGA)